

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

RAMANI YA WILAYA YA BAHI



RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU WILAYA YA BAHI
TAREHE 18-19/08/2019

NA	TAREHE	MUDA	MAHALI NA UMBALI	SHUGHULI	MUHUSIKA
1.	18/08/2019	2:00-2:30	MAYAMAYA/ZAMAHERO	Makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru.	Mkuu wa Wilaya.
2.		2:30	MAYAMAYA KM.1	Kuondoka eneo la mapokezi kuelekea eneo la mradi wa utunzaji wa chanzo cha maji na uhifadhi wa msitu.	Mkuu wa Wilaya.
3.		2:40-2:50	MAYAMAYA	Kuwasili eneo la mradi :- • Kupata taarifa na kutembelea mradi wa utunzaji wa chanzo cha maji na uhifadhi wa msitu wa Chenene.	Mkuu wa Wilaya. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
4		2:50	MAYAMAYA KM.10	Kuondoka eneo la mradi na kuelekea Zanka.	Mkuu wa Wilaya.
5		3:00-3:10		• Kuwasili Zanka na kukimbiza mita 200.	Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru.
6		3:10	KM.15	Kuondoka zanka na kuelekea Mundemu.	Mkuu wa Wilaya.
7.		3:25-3:40	MUNDEMU	Kuwasili Mundemu na:- • Kupata maelezo ya shughuli za mapambano dhidi ya Rushwa kutoka kwa wanafunzi wa Mundemu Sekondari. • Kuzindua mradi wa Umaliziaji wa maboma ya madarasa manne Sekondari Mundemu.	Mkuu wa Wilaya. Mkurugenzi Mtendaji. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
8.		3:40	MUNDEMU	Kuondoka shule ya	Mkuu wa Wilaya.

NA	TAREHE	MUDA	MAHALI NA UMBALI	SHUGHULI	MUHUSIKA
			KM.4.5	sekondari Mundemu kuelekea viwanja vya mahakama Mundemu.	
9.		3:50-4:00	MUNDEMU	Kuwasili Viwanja vya mahakama ya mwanzo Mundemu • Kutoa Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru	Mkuu wa Wilaya. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
10.		4:00-4:20	MUNDEMU	CHAI	Kamati ya chakula
11.		4:20	MUNDEMU Km.1	Kuondoka eneo la chai kuelekea eneo la kiwanda cha kokoto cha kampuni ya KASCCO Mining Limited Mundemu	Mkuu wa Wilaya.
12.		4:25-4:35	MUNDEMU	Kuwasili Kwenye kiwanda :- • Kuweka jiwe la msingi mradi wa kuzalisha kokoto.	Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
13		4:35	MUNDEMU Km.17.7	Kuondoka eneo la mradi wa kiwanda cha uzalishaji kokoto KASCCO kuelekea Ilindi	Mkuu wa Wilaya.
14.		4:50-5:00	ILINDI	Kuwasili Ilindi :- • Kutoa Salaam za Mwenge wa Uhuru	Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
15.		5:00	ILINDI Km.16.6	Kuondoka Ilindi na kuelekea Ibihwa kupitia Msembeta.	Mkuu wa Wilaya.
16.		5:30-6:00	IBIHWA	Kuwasili Ibihwa na:- • Kuzindua hamasa na kupata maelezo mafupi jinsi Wilaya ilivyojipanga katika kuhamasisha Uchaguzi wa Serikali za	Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.

NA	TAREHE	MUDA	MAHALI NA UMBALI	SHUGHULI	MUHUSIKA
				Mitaa.	
17.		6:00	IBIHWA Km.21.1	Kuondoka Ibihwa kuelekea Bankolo kupitia Munkola .	Mkuu wa Wilaya.
18.		6:50-7:10	BANKOLO	Kuwasili Bankolo :- • Kutoa Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru.	-Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
19.		2:10-8:00		CHAKULA CHA MCHANA	Kamati ya chakula
20.		8:00	BANKOLO Km.13.4	Kuondoka Bankolo kuelekea Mkakatika.	Mkuu wa Wilaya.
21.		8:15-8:30	MKAKATIKA	Kuwasili Mkakatika :- • Kuweka jiwe la msingi mradi wa usambazaji maji kijiji cha Mkakatika.	-Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
22.		8:30	MKAKATIKA Km.3	Kuondoka Mkakatika kuelekea Bahi.	Mkuu wa Wilaya.
23.		8:50-9:20	BAHI	Kuwasili Bahi :- • Kutembelea na kupata taarifa ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bahi.	-Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
24.		9:20	BAHI Km.2	Kuondoka eneo la mradi wa Hospitali ya Wilaya kuelekea Bahi Mwanachugu.	Mkuu wa Wilaya.
25.		9:30-9:45	BAHI	Kuwasili Bahi Mwanachugu • Kuweka jiwe la msingi barabara za mji wa Bahi zenye urefu wa KM.2.3	-Mkuu wa Wilaya. -Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
26.		9:45	BAHI Km.1.9	Kuondoka kwenye mradi wa barabara na kuelekea kwenye mradi wa Kituo cha ukaguzi wa mifugo.	Mkuu wa Wilaya.
27.		9:45-10:00	BAHI	Kuwasili kwenye Mradi :- • Kuzindua mradi wa kituo cha ukaguzi wa mifugo.	Mkuu wa Wilaya. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.

NA	TAREHE	MUDA	MAHALI NA UMBALI	SHUGHULI	MUHUSIKA
28.		10:00	BAHI Km.1.2	Kuondoka Kituo cha Ukaguzi wa mifugo na kuelekea eneo la mkesha.	Mkuu wa Wilaya.
29.		10:10-	BAHI	Kuwasili Eneo la mkesha; • Kukagua na kupata maelezo ya shughuli za Uchaguzi wa srikali za mitaa. • Kupata maelezo ya shughuli za mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI na Malaria. • Kupata maelezo ya shughuli za mapambano dhidi ya Rushwa kutoka TAKUKURU. • Kupata maelezo ya shughuli za mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kutoka kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari Bahi. • Kupata maelezo ya kukagua shughuli za vikundi vya vijana wenye ulemavu na wanawake. • Kusoma Risala ya Wilaya. • Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru.	Mkuu wa Wilaya. Mkurugenzi Mtendaji. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
				CHAKULA CHA JIONI.	Kamati ya chakula.
					Mkuu wa Wilaya.

NA	TAREHE	MUDA	MAHALI NA UMBALI	SHUGHULI	MUHUSIKA
				• Mkesha wa Mwenge wa Uhuru.	Mkurugenzi Mtendaji. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru.
30.	19/08/19	12:00-12:35	BAHI	CHAI YA ASUBUHI.	Kamati ya chakula.
		12:35-1:00	BAHI	Kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mhe.Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.	Mkuu wa Wilaya Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru..
31.		1:00	BAHI KM 75	Kuondoka Bahi kuelekea k ijiji cha Sanza Wilaya ya Manyoni,Mkoani Singida.	Mkuu wa Wilaya.
32.		2:00-2:30	SANZA-MKOANI SINGIDA.	Kuwasili Sanza na • Kukabidhi Mwenge wa Uhuru Mkoani Singida	Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

RISALA YA UTII YA WANANCHI WA WILAYA YA BAHI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI WAKATI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU TAREHE 18/08/2019

1.0. UTANGULIZI:

Mheshimiwa Rais;
Sisi wananchi wa Wilaya ya Bahi tunayo furaha kubwa isiyo na kifani kuupokea *Mwenge wa Uhuru* , ikiwa leo ni siku ya 139 tangu mbio za *Mwenge wa Uhuru* zilizozinduliwa rasmi tarehe **02/04/2019** katika Mkoawa **Songwe** na **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.**

Tunawakaribisha kwa furaha kubwa wakimbiza *Mwenge wa Uhuru* katika Wilaya yetu yenye Tarafa **4,** Kata **22**, vijiji **59**,vitongoji **553**,eneo la kilometa za mraba **5,948** najumla ya watu **221,645** (wanaume **105,975** *(47.8%)* na wanawake **115,670** (*52.2 %)* kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Rais;
Sisi wananchi wa Wilaya ya Bahi tunaamini kwamba *Mwenge wa Uhuru* ni ishara ya kuleta **Utulivu, Amani, Upendo**, **Umoja na Mshikamano** wa Kitaifa baina ya watanzania. Aidha;Tunaamini pia kwamba, *Mwenge wa Uhuru* ni kichocheo cha wananchi kujiletea maendeleo yao kwa njia ya kujitegemea. Lakini pia ni nafasi nzuri ya kuwajulisha na kuwaonesha wananchi juhudi zinazofanywa na Serikali yao katika kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Rais;
Uchumi wa Wilaya unatokana na kilimo na ufugaji. Makadirio ya pato la mkazi kwa mwaka 2007 yalikuwa shilngi **206, 000.**Kwa sasa inakadiriwa pato hili kuongezeka hadi kufikia shilingi **427, 489** sawa na ongezeko la **207.5%.**
Hali ya kisiasa ni shwari ambapo tuna vyama 7 vya siasa vinavyofanyakazi ambavyo ni CCM, CUF, SAU, CHADEMA, TLP, NCCR- Mageuzi na ACT –Wazalendo. Aidha, hali ya ulinzi na usalama ni shwari na vyombo vyote vya dola kwa pamoja vinatimiza wajibu wake.

2.0 UTEKELEZAJI WA UJUMBE WA *MWENGE WA UHURU* MWAKA 2019

Ujumbe Mkuu wa *Mwenge wa Uhuru* mwaka huu ni;

2.1*. "Maji ni haki ya kila Mtu, Tutunze vyanzo vyake na tukumbuke kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa"*

Mheshimiwa Rais;
Katika kuhakikisha ujumbe wa *Mwenge wa Uhuru* unazingatiwa, Wilaya inaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa wananchi wanatunza vyanzo vyote vya maji kwa kutoharibu mazingira na kwa kutofanya shughuli za uzalishaji hasa kilimo kwenye vyanzo vya maji.Lakini pia kutokata miti na uchomaji misitu. Aidha;Wilaya imeendelea na jukumu lake la kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama umbali usiozidi mita **400** kama ilivyoainishwa na sera ya taifa ya maji ya mwaka 2002.Hadi kufikia Juni,2019 idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji safi na salama ni **134,500** sawa na **54.7%** ya wakazi wote waishio vijijini katika wilaya yetu.

Mheshimiwa Rais;

Wilaya imeendelea kutekeleza Programu ya **Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini** . Programu hii, awamu ya kwanza ilihusisha usanifu na ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji vya Nondwa, Mchito, Nholi, Zanka, Mindola, Chiguluka, Nghulugano, Chimendeli, Mundemu na Nguji. Miradi hii ilishakamilika na inafanya kazi. Jumla ya shilingi **4,024,508,224.71** zilitumika na wanufaika ni watu **50,000**. Pia utekelezaji wa **Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini awamu ya**

pili(WSDP II) na Quickwin, Wilaya inaendelea kutekeleza miradi mipya **2** katika vijiji vya Mkakatika (umefikia **60%)** na Magaga **40%**). Aidha;Uchimbaji wa visima virefu umekamilika katika vijiji vya Mpamantwa, Ibihwa, Bahi Makulu, Ikumbulu, Lamaiti, Chali Igongo, Chali Isangha,Zejele,Chimendeli,Chikola na Lukali.

Mheshimiwa Rais;
Idadi ya watu katika makao makuu ya Wilaya inakadiriwa kufikia **12,207** kwa mwaka 2018/2019. Hali ya upatikanaji wa maji makao makuu ya Wilaya bado si wa kutosha. Mahitaji ya maji ni lita **1,222,200** kwa siku na wastani wa maji yanayozalishwa ni lita **216,000** kwa siku, idadi ya watu wanaopata maji ni **2,197** sawa na **18%.**

Mheshimiwa Rais;
Katika kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wilaya imefanya uhakiki wa maeneo ya kiutawala ambapo Wilaya ina vijiji **59** na vitongoji **553** vinavyotarajia kufanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019.Kama wilaya tunaendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019.Aidha;Tumeandaa vipeperushi vyenye ujumbe wa kutoa elimu ya Uchaguzi na kuvisambaza maeneo mbalimbali ndani ya Wilaya.

Ujumbe wa Kudumu wa *Mwenge wa Uhuru*
2.2 MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI; Chini ya kauli mbiu **"*Pima, Jitambue,Ishi"***

Mheshimiwa Rais
Kwa kutambua kuwa UKIMWI ni janga la Taifa, Wilaya inafanya jitihada mbalimbali ili kunusuru kizazi kilichopo na kijacho. Huduma zitolewazo ni upimaji wa Virusi vya Ukimwi kwa hiari na unasihi (CITC) katika vituo **43**, kutoa huduma kwa watu waishio na VVU (CTC) katika vituo **6** na huduma matembezi **2** sanjari na kutoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) zinazotolewa katika vituo **42.**

Mheshimiwa Rais **;**
Katika jitihada za kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI, Wilaya kwa kushirikiana na wadau wengine wa mapambano dhidi ya UKIMWI (NGO's na mashirika ya dini) imeendelea kuhamashisha wananchi katika upimaji wa hiari sanjari na kuendelea kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI katika vituo **6** (Vituo va Afya **5** na Zahanati **1**) ambavyo ni Bahi, Chipanga, Mtitaa, Mundemu, Kigwe na Babayu. Katika kufuatilia **afua za UKIMWI** tumeweza kukutana na kamati **5** za UKIMWI za kata za Mundemu,Msisi,Babayu,Zanka na Chikola ambapo zimejengewa uwezo juu ya utendaji wao wa kazi. Katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Desemba, 2018, jumla ya watu **23,677** wamepima VVU na kati yao wanawake ni **15,685** na wanaume ni **7,992**. Miongoni mwao waliopatikana na VVU ni **622** (wanaume **204** na wanawake **418**) sawa na **2.6%** ya maambukizi kiwilaya.Hii inaonesha kiwango cha maambukizi kupungua kutoka **3.6%** mwaka 2016 na kufikia **2.6%.** Aidha;Katika kipindi hicho Wilaya imekuwa na jumla ya watu wanaoishi na maambukizi ya VVU (WAVIU) **5,685**. Kati yao wanaume ni **1,627** na wanawake ni **4,058.**

Mheshimiwa Rais;
Katika kutoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT),kwa kipindi hicho wajawazito waliohudhuria kliniki ni **11,272**,nawote walipimwa VVU ambapo **150** walikutwa na VVU sawa na **1.3 %** ya waliopimwa.

Mheshimiwa Rais;
Sisi na wananchi wa wilaya ya Bahi kwa umoja wetu tunaunga mkono kwa dhati mapambano dhidi ya UKIMWI ili kuhakikisha ***"Tanzania bila Maambukizi mapya,Unyanyapaa na Vifo vitokanavyo na UKIMWI; Inawezekana ifikapo 2030"*.**

2.3 MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA; Chini ya kauli mbiu **"*Nipo tayari kutokomeza Malaria, Wewe Je* ?."**

Mheshimiwa Rais;
Kama zilivyo sehemu nyingine za Nchi yetu, wilaya ya Bahi ni miongoni mwa wilaya zinazoathirika na ugonjwa wa malaria. Hivyo;Juhudi za makusudi zinaendelea kufanyika kwa kuelimisha jamii kwenye mikutano ya hadhara,kutumia mabango,magari ya matangazo na kugawa vipeperushi mbalimbali vinavyoelezea umuhimu wa kutumia vyandarua vyenye dawa ya viuatilifu vya muda mrefu viuwayo mbu waenezao malaria,matumizi sahihi ya dawa Mseto za malaria,kuhimiza tabia ya kutibiwa mapema ,matumizi ya dawa za kuzuia malaria kwa kina mama wajawazito na kunyunyizia dawa za kuua viluilui vya malaria sehemu za mazalia ya mbu.Aidha;Kwa kipindi cha Julai,2018 hadi Juni,2019 vyandarua **9,374** sawa na **97.7%** vimegawiwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano sanjari na kupatiwa chanjo ya surua(Rubella) ya kwanza wanapotimiza miezi sita. Lakini pia akina mama wajawazito **12,096** wanaohudhuria hudhurio la kwanza kwenye vituo vyote vya huduma za afya wamegawiwa vyandarua sawa na **98.3%** katika kipindi hiki. Mkakati wa unyunyiziaji dawa ya viuadudu umetumika ili kudhibiti mbu waenezao malaria ambapo ulifanyika kwenye ukubwa wa mita za mraba **165,158** katika maeneo ambayo yana mazalia ya mbu na lita **2,800** za dawa zimetumika.

Mheshimiwa Rais;
Wananchi wa wilaya ya Bahi tumeweza kushiriki kikamilifu na kutoa hamasa kwa jamii namna ya kujikinga na malaria kwa kushirikiana na wadau wa **TCDC** (Tanzania Communication Development Centre) ambao walisaidia kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo matamasha katika kata **16** yaliyobeba ujumbe mbalimbali za kuelekeza jinsi ya kujikinga na malaria.Pia wadau hawa walitumia gari kubwa la matangazo lililokuwa likipita vijijini kutoa elimu kwa jamii na takribani watu **27,010** waliweza kupatiwa elimu hii kwa kipindi hicho cha maadhimisho ya siku ya malaria duniani Aprili,2019.
Aidha; Kwa kipindi cha Julai,2018 hadi Juni,2019 watu **59,416** walipimwa malaria na waliokutwa na vimelea ni **7,000 s**awa na **11.7%** na wote walipata matibabu sanjari na kupewa elimu ya kujikinga na Malaria.Lakini pia wilaya inaendelea kuhamasisha jamii kujiunga na Bima ya Afya ili kukabiliana na gharama za matibabu ambapo hadi sasa kaya **1,273** zimejiunga na Bima ya Afya (CHF) kati ya lengo la kaya **14,776**.

2.4 MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA; Chini ya kauli mbiu
"Tujenge Maisha Yetu,Jamii Yetu na Utu Wetu Bila Dawa za Kulevya".

Mheshimiwa Rais;
Wilaya ya Bahi kwa kuzingatia mpango wa Taifa wa Kudhibiti Dawa za Kulevya wa mwaka 2002, imeendelea na jitihada za kupambana na biashara na matumizi haramu ya dawa za kulevya. Kwa kutambua athari za dawa za kulevya kwa watoto na vijana wetu ambao ndio tegemeo na nguvu kazi ya taifa, Wilaya imeendelea kutekeleza ***Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka2007*** kwa kuwahamasisha vijana kuunda vikundi vya kiuchumi kama njia ya kujiongezea kipato na kujiepusha na athari za matumizi ya dawa za kulevya. Mpaka sasa kuna vikundi **151** vya vijana ambavyo vinajishughulisha na kazi mbalimbali za kujiletea maendeleo. Hivyo wilaya inatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya *Mwenge wa Uhuru* inayosema ***"Tujenge Maisha Yetu, Jamii Yetu na Utu Wetu Bila Dawa za Kulevya".***

Mheshimiwa Rais;
Tatizo la dawa za kulevya kwa wilaya ya Bahi si kubwa sana. Wapo baadhi ya vijana wachache wanaojihusisha na uvutaji wa bangi. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai,2018 hadi Juni,2019 jumla ya kesi **5** za kupatikana na bangi kinyume cha sheria zimefikishwa mahakamani ambapo kesi **2** zinaendelea kusikilizwa, kesi **2** zimetolewa hukumu na watuhumiwa wamepatikana na hatia kwa kufungwa ama kutozwa faini na kesi **1** watuhumiwa wameachiwa huru baada ya ushahidi kukosekana.

2.5MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA; Chini ya kauli mbiu ***"Kataa Rushwa – Jenga Tanzania".***

Mheshimiwa Rais;
Wilaya ya Bahi kwa kuzingatia **sheria ya kupambana na rushwa Na. 11ya mwaka2007** imeendelea kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuzuiamianya ya rushwa na kuwasihi wananchi kujiepusha na vitendo vya rushwa. Sisi Wananchi wa wilaya ya Bahi tunatambua kuwa mapambano dhidi ya rushwa ni kazi ya kila raia, hivyo tunaunga mkono kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru mwaka huu 2019 inayosema ***"Kataa Rushwa – Jenga Tanzania"***

Mheshimiwa Rais;
Wilaya yetu kupitia **TAKUKURU** imepata mafanikio makubwa katika kutekeleza mapambano dhidi ya rushwa kupitia Elimu kwa umma ambapo jumla ya mikutano **25**,semina **19** katika maeneo mbalimbali, ufunguzi na uimarishaji wa klabu **84** za kupambana na rushwa zilifanyika na ugawaji wa vipeperushi **3,150.**Kuanzia Julai,2018 hadi Juni,2019 **TAKUKUR**U imepokea taarifa **43** za kuwepo kwa vitendo vya rushwa katika taasisi Mbalimbali za Serikali na Halmashauri ya Wilaya; majalada ya uchunguzi yaliyokamilika yapo **4**. **TAKUKURU** inaendelea kuelimisha taasisi na jamii kwa ujumla juu ya **Sheria ya kupambana na Rushwa.**Jumla ya miradi **10** ya maendeleo katika sekta za Afya, mifugo, elimu,ujenzi na maji inayotekelezwa imefanyiwa ufuatiliaji kuanzia ngazi za awali mpaka utekelezaji wake. Aidha kesi mpya **4** zimefunguliwa mahakamani.

Mheshimiwa Rais;
Katika jitihada za Wilaya kupinga vitendo vya rushwa, kila Ofisi imebandika bango la tahadhari "**Ndugu mteja huduma ni haki yako usitoe wala kupokea Rushwa"**

Aidha mikakati ya kupambana na rushwa imekuwa ni pamoja na kusimamia na kutekeleza sheria mpya ya manunuzi ambayo imetoa wigo mpana kwa wawakilishi wa wananchi kuhakiki mwenendo mzima wa kutoa zabuni. Kutolewa elimu kwa waajiriwa wapya kuichukia rushwa na kutoa taarifa kupitia namba za simu za viongozi wa ngazi ya Wilaya pindi wanapohisi dalili za vitendo vya rushwa.

3.0 VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI/KIUCHUMI

Mheshimiwa Rais;
Katika kutekeleza sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia yamwaka2000**,** Sera ya maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 na Sera ya Taifa ya Vijana yamwaka 2007,Wilaya ya Bahi imefanikiwa kuunda jumla ya vikundi **508** vya kiuchumi ambapo Vikundi **172** ni vya mchanganyiko, Vikundi vya vijana **151,** Vikundi vya wanawake **179** na Walemavu **6**.

3.1. UIMARISHAJI WA VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI *VYA* WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAU

Mheshimiwa Rais;
Wilaya inaendelea kuwezesha vikundi kwa Mitaji, Vifaa, Mafunzo na Elimu ya Ujasiriamali. Katika kutekeleza agizo la Serikali la kutoa **10%** ya mapato ya ndani kwa Vikundi vya wanawake,vijana na walemavu,kwa mwaka 2018/19,Halmashauri ilitenga Shilingi **115,779,400** kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na walemavu. Fedha hizi ni **10%**ya makadirio ya mapato halisi ya ndani (**sh**.**1,157,794,000).** Hadi kufikia Juni 2019, Halmashauri imeweza kutoa kiasi cha shilingi **54,000,000** kwa vikundi **38** (Wanawake sh.**27,100,000** kwa vikundi **21**,vijana sh.**18,400,000** kwa vikundi **11** na walemavu sh. **8,500,000** kwa vikundi **6**).Kwa mwaka ujao wa fedha2019/2020Halmasahauri imetengaShilingi **122,701,189.60.**

4.0 MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA ELIMU, AFYA, UJENZI, KILIMO, MIFUGO, UKUSANYAJI WA KODI/MAPATO, HUDUMA ZA JAMII, ULINZI NA USALAMA WA RAIA NA MALI ZAO.

Mheshimiwa Rais;
Hali ya Ulinzi na Usalama ipo shwari katika maeneo yetu yote na vyombo vyote vya dola kwa pamoja vinatimiza wajibu wake,hivyo wananchi kuendelea kufanya shughuli za uzalishaji mali bila hofu. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 katika sekta ya elimu kupitia"*Elimu bila Malipo*" hadi kufikia mwezi Juni,2019,Wilaya imepokea shilingi **769,051,689.80 (**shilingi **249,037,052** kwa sekta ya elimu sekondari na **520,014,637.80** kwa sekta ya elimu msingi.Wilaya pia imepokea fedha za motisha (Lipa kulingana na matokeo-P4R) shilingi **263,800,000** (shilingi **115,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa bweni na madarasa 2 katika shule ya Sekondari Mwitikira na shilingi **148,800,000** kwaShule za msingi za Ilindi Mgondo,Mchito,Mindola,Isangha na Sokoine). Aidha;Tumepokea shilingi **362,500,000** kutoka serikali kuu ikiwa ni fedha za ukamilishaji wa maboma **29** ya madarasa katika shule za sekondari **15**,hivyo kufanya mazingira ya kujifunzia na kufundishia kuwa rafiki kwa wanafunzi na walimu. Lakini pia, wilaya imeweza kuboresha miundombinu ya barabara kwa kupokea fedha kiasi cha shilingi **1,022,210,000** kati ya shilingi **1,398,980,000**kupitia bajeti yake ya mwaka 2018/19 ambapo miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Kwa upande wa Afya tumepokea kiasi cha shilingi **1,500,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Rais;
Halmashauri ya wilaya ilikisia kukusanya mapato halisi ya ndani shilingi **1,157,794,000** na mapato ya kisekta shilingi **710,250,000** na kufanya jumla ya makisio kuwa kiasi cha shilingi **1,868,044,000**. Hadi kufikia tarehe 30/06/2019,Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi **1,460,628,830** sawa na **78 %** ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo,**mapato halisiya ndani** ni shilingi **957,158,638** sawa na **83%,**na **mapato ya kisekta** ni shilingi **503,470,192** sawa na **71%** ya lengo**.** Aidha;Halmashauri inakusanya mapato yake kwa kutumia mashine za kieletroniki (POS) ambapo mpaka sasa inazo jumla ya mashine **70** . Kati yake, **59**zinazotumika katika vijiji vyote 59, **5** kwenye kata, **2** kwenye mageti, **3** timu ya mapato ya Wilaya na **1** inatumiwa na msimamizi wa mfumo.

Mheshimiwa Rais;
Katika kubuni kuongeza vyanzo vya mapato Wilaya imeandika maandiko mawili ambayo ni **Ujenzi wa Kiwanda cha ngozi** na **Ujenzi wa Stendi ya mabasi na Maegesho ya malori** ambapo tunatarajia kukusanya kiasi cha shilingi **925,684,887**(kiwanda cha ngozi shilingi**546,154,887** na stendi shilingi **379,530,000**) kwa mwaka,miradi hii ikijengwa na kuanza kufanya kazi.

5.0 MIRADI YA MWENGE.

Mheshimiwa Rais;
Mwenge wa Uhuru mwaka2018ulifungua, ulikagua na kuweka mawe yamsingi kwenye miradi **6** yenye thamani ya shilingi **1,864,831,735.** Kwa mwaka 2019*Mwenge wa Uhuru* umefanikiwa kuweka mawe ya msingi, kuzindua na kukagua miradi **7** yenye thamani ya shillingi **8,717,470,283.77.**Kati ya fedha hizi nguvu za wananchi ni shilingi **5,039,709,150** Serikali kuu shililingi **3,608,032,813.77**,Halmashauri shilingi **12,328,320** na Wadau wa maendeleo shilingi **57,400,000**.
NB: *Taarifa ya kila mradi imeambatishwa*.

6.0MICHANGO YA MWENGE:

Mheshimiwa Rais;
Mwaka 2018 wananchi wa wilaya ya Bahi walichangia jumla ya shilingi **12,657,500**. Kati ya fedha hizo, shilingi **8,227,375** zilitumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za *mwenge wa Uhuru* na shilingi

4,430,125 zilitumika kugharimia miradi ya maendeleo ya wananchi. Kwa mwaka 2019 wananchi wamechangia jumla yashilingi**16,950,000** Kati ya fedha hizi wilaya imechangia shilingi**15,450,000**kufanikisha sherehe za *Mwenge wa UhuruKimkoa* na shilingi **1,500,000** zimetumika kwenye mradi wa pakilio la mifugo kijiji cha Bahi Sokoni.

7.0 UENDELEVU WA MIRADI ILIYOZINDULIWA /KUWEKEWA JIWE LA MSINGI NA *MBIO ZA MWENGE WA UHURU* KWA MWAKA 2017 NA 2018

Kwa mwaka 2017 na 2018 jumla ya miradi **13** ilipitiwa na *Mwenge wa Uhuru*. Kati yake miradi **7** ilizinduliwa,**3** ilikaguliwa na **3** iliwekewa mawe ya msingi. Miradi iliyowekewa mawe ya msingi,**2**imekamilika inatoa huduma iliyokusudiwa na **1** uko hatua za ukamilishaji. Lakini pia miradi yote iliyozinduliwa na iliyokaguliwa inaendelea kutoa huduma.

8.0 HITIMISHO:

Mheshimiwa Rais;
Tunampongeza kiongozi wa mbio za *Mwenge wa Uhurukitaifa* na msafara wake kwa kazi kubwa walioifanya ya kuweka mawe ya msingi,kufungua na kukagua miradi ya maendeleo katika wilaya yetu.
Pia tunawatakia kheri na baraka za Mwenyezi Mungu na Afya njema wakimbiza Mwenge wote katika kutekeleza na kukamilisha jukumu hili muhimu la kizalendo kwa ustawi na uhai wa Taifa letu.

"Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania"
MWENGE WA UHURU HOYEE !!!!

Kwa niaba ya wananhi wa Wilaya ya Bahi

Mwanahamisi Munkunda,
Mkuu wa Wilaya ya Bahi

Saini/Muhuri……
Tarehe 18/08/2019

WILAYA YA BAHI

KIAMBATISHO "A"

TAARIFA YA UWEZESHAJI KIUCHUMI KWA WATU WENYE ULEMAVU (2%) YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI

Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ilitarajia kukusanya jumla ya shillingi 1,157,794,000/= yakiwa ni mapato halisi ya ndani. Kati ya fedha hizi jumla ya shilingi 23,155,880/=ikiwa ni 2% zilitengwa kwa ajili ya kuwawezesha walemavu. Hadi kufikia Juni,2019, jumla ya shilingi **8,500,000/=,** ziliweza kukopeshwa kwa vikundi vya walemavu, kiasi ambacho ni sawa na 44.4 % ya lengo. Kiasi hiki kilitolewa kutokana na mapato halisi ya ndani ambayo hadi Juni,2019 yalikuwa ni shilingi **957,158,638/=.**

MWAKA	JINA LA KIKUNDI	MAHALI WANUFAI KA WALIPO	AINA YA MIRADI INAYOTEK ELEZWA	IDADI YA VIKUNDI/W ATU WALIONUFAI KA	KIASI KILICHOTOL EWA (Shs.)
2018/2019	Tumaini Group	Lamaiti	Ufugaji, biashara ya kuku, uuzaji wa batiki, biashara ya asali.	Watu 5	4,000,000
	Kikundi Cha Upendo Wa Njiwa	Bahi	Ujasiriamali wa samaki, mchele na biashara ndogo ndogo	Watu 5	1,000,000
	Kikundi Cha Walemavu Nkogwa	Bahi Sokoni	Biashara ndogo ndogo	Watu 5	500,000
	Uwawaki Group	Kigwe	Ujasiriamali mdogo mdogo	Watu 5	1,000,000
	Amkeni Wanawake Viziwi	Kigwe	biashara ndogo ndogo	Watu 6	1,000,000
	Twende Sawa	Bahi Sokoni	Kununua nafaka na kuuza	Watu 7	1,000,000
	Jumla			**Watu33(viku ndi 6)**	**8,500,000**

KIAMBATISHO "B"

TAARIFA YA UWEZESHAJI KIUCHUMI KWA VIJANA (4%) YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI – 2018/2019

Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ,Halmashauri ya wilaya ya Bahi ilitenga jumla ya shilingi 46,311,760/=zikiwa ni 4% ya makisio ya mapato halisi ya ndani (sh.1,157,794,000/=) kwa ajili ya kuwawezesha vijana.Hadi kufikia Juni,2019, jumla ya shilingi 18,400,000/=, ziliweza kukopeshwa kwa vikundi vya vijana kiasi ambacho ni sawa na 48 % ya lengo. Kiasi hiki kilitolewa kutokana na mapato halisi ya ndani ambayo hadi juni,2019 yalikuwa ni shilingi 957,158,638/=

MWAKA	JINA LA KIKUNDI	MAHALI WAUFAIKA WALIPO	AINA YA MIRADI INAYOTEKELEZWA	IDADI YA VIKUNDI/WATU WALIONUFAIKA	KIASI KILICHOTOLEWA (Shs.)
	Tenge Mitindo	Bahi Sokoni	Ushonaji	Watu 5	1,000,000
2018/2019	Bodaboda	Mpalanga	Ushonaji ufugaji kuku, usafirishaji	Watu 6	1,000,000
	Wanambo ni	Ilindi	Ushonaji, utengenezaji wa sabuni, kilimo na batiki	Watu 10	2,000,000
	Women Developm ent Group	Nagulo Bahi	Utengenezaji wa sabuni ya maji, unga wa lishe na biashara ndogondogo	Watu 15	1,500,000
	Hapa Kazi	Bahi Sokoni	Ujasiriamali wa kununua mpunga na kuuza mchele na kilimo	Watu 5	900,000
	Tumaini Group Bankolo	Bankolo	VICOBA na ushonaji	Watu 14	2,000,0000
	Kikundi Cha Vijana Mundemu	Mundemu	Usindikaji wa alizeti, kilimo na vikoba	Watu 10	5,000,000
	Msopo Workshop	B/Sokoni	Kutengeza samani na ufundi chuma,	Watu 8	1,500,000
	Kikundi Cha Kazi	Mkakatika	Ufundi Seremala,ufugaji wa	Watu 7	1,500,000

MWAKA	JINA LA KIKUNDI	MAHALI WAUFAIKA WALIPO	AINA YA MIRADI INAYOTEKELEZWA	IDADI YA VIKUNDI/WATU WALIONUFAIKA	KIASI KILICHOTOLEWA (Shs.)
	Kwanza		kuku na vikoba		
	Kikundi cha Youth Pride Networ	Ilindi	Ufugaji kuku wa kiasili na kilimo cha mbogamboga	Wau 5	1,000,000
	Wasaka tonge	Bahi Sokoni	Kuosha pikipiki na magari,duka la nguo na ushonaji	Watu 6	1,000,000
	Jumla			**Watu 91 (Vikundi 11)**	**18,400,000**

KIAMBATISHO "C"

TAARIFA YA UENDELEVU WA MIRADI ILIYOPITIWA NA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017 NA 2018

MWAKA	NA.	JINA LA MRADI	KUZINDULIWA/ KUWEKEWA JIWE LA MSINGI KUKAGULIWA	HALI YA UENDELEVU WA MRADI
2017	1.	Kukagua na kupata maelezo kutoka kwenye vikundi vya uzalishajimali vya wanawake na vijana-Mundemu	Kukaguana kupata maelezo	Vikundi vyote vinne vinaendelea na shughul izao 1.**Mkombozi Group(**mchanganyiko**)**-wafugaji nyuki na kurina asali 2.**Umoja Group**(wanawake-Mama lishe) – wanaendelea kupata tenda katika matukio mbalimbali ya jamii**-**semina,mikutanona mafunzo mablimbali jamii3.**Nyemo** (wanawake**-**VIKOBA) – kinaendelea vizuri 4.**Wanambon**i(Vijana)-wanaendelea na ushonaji
	2.	Kuzindua nyumba za walimu wa Sekondari Msisi juu.	Kuzindua	Nyumba zinatumika

MWAKA	NA.	JINA LA MRADI	KUZINDULIWA/ KUWEKEWA JIWE LA MSINGI KUKAGULIWA	HALI YA UENDELEVU WA MRADI
	3.	Kuzindua mradi wa usambazaji maji kijijini Mchito.	Kuzindua	Mradi unaendelea kutoa huduma.
	4.	Kuzindua mitambo ya kusukuma maji kwenda shambani na kukabidhi hati miliki ya shamba la LUBALA kijiji cha Lamaiti	Kuzindua	Mradi unaendelea kutoa huduma
	5.	Mradi wa Uchakataji na Utengenezaji wa asali na kukabidhi hati miliki ya shamba kwa kikundi cha UKILA katika kijiji cha Lamaiti	Kukagua	Mradi unaendelea vizuri
	6.	Kuzindua kiwanda kidogo cha mwananchi cha Ufundi chuma na uselemalaKijiji cha Ibihwa	Kuzindua	Kiwanda kinaendelea na uzalishaji.
	7.	Kuweka jiwe la msingi Daraja la Nghulugano.	Kuweka jiwe la msingi	Daraja limekamilika na linatumika.
2018	1.	Mradi wa shamba la mikorosho Kijiji cha Chibelela	Kukagua na kupata maelezo	Mradi unaendelea vizuri
	2.	Mradi wa ujenzi wa nyumba ya Walimu (1 kwa 6)Mpalanga	Kuweka jiwe la msingi	Ujenzi umefikia hatua za mwisho za ukamilishaji.
	3.	Mradi wa mwananchi wa kiwanda kidogo cha kusindika nafaka kijiji cha Kigwe	Kuzindua	Kiwanda kinafanya kazi.
	4.	Mradi wa ujenzi wa ofisi ya TANESCO Wilaya ya Bahi	Kuzindua	Ofisi inatumika.
	5.	Mradi wa uboreshaji wa kituo cha Afya Bahi	Kuweka jiwe la msingi	Uboreshaji umekamilka na kituo kinaendelea kutoa huduma
	6.	Mradi wa usambazaji Maji wa Bahi	Kuzindua	Mradi unaendelea kutoa huduma

Mwanahamisi Munkunda,
Mkuu wa Wilaya ya Bahi

Saini/Muhuri……..
Tarehe 18/08/2019

KIAMBATISHO "D"

WILAYA YA BAHI

ORODHA YA MIRADI ITAKAYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2019 PAMOJA NA THAMANI YAKE

NA	JINA LA MRADI	MAHALI ULIPO / KIJIJI	SHUGHULI	S/KUU (TSh.)	H/W (TSh.)	WANANCHI (TSh.)	WADAU/ WAFADHILI (TSh.)	THAMANI (TShs)
1.	Utunzaji wa chanzo cha maji na uhifadhi wa msitu wa Chenene.	Mayamaya	Kutembelea mradi	-	-	-	27,400,000.00	27,400,000.00
2.	Ujenzi wa maboma ya vyumba vinne vya madarasa	Mundemu	Kuzindua	50,000,000	-	30,000,000.00	-	80,000,000.00
3.	Kiwanda cha uzalishaji wa kokoto Kampuni ya KASCCO Mundemu	Mundemu	Kuweka jiwe la Msingi			5,000,000,000.00		5,000,000,000.00
4.	Usambazaji wa maji kijiji cha Mkakatika	Mkakatika	Kuweka jiwe la msingi	637,897,271.40	5,440,320.00	3,209,150.00	-	646,546,741.40
5.	Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya	Bahi Sokoni	Kutembelea na kupata taarifa ya maendeleo ya ujenzi.	1,500,000,000.00	-	6,500,000.00	-	1,506,000,000.00
6.	Ujenzi wa barabara za lami KM 2.3 mji wa Bahi	Bahi Sokoni	Kuweka jiwe la msingi	1,420,135,542.37	-	-	-	1,420,135,542.37
7.	Ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa mifugo Bahi	Bahi Sokoni	Kuzindua	-	6,888,000.00	-	30,000,000.00	36,888,000.00
	JUMLA KUU			**3,608,032,113.77**	**12,328,320**	**5,039,709,150**	**57,400,000**	**8,717,470,283.77**

KIAMBATISHO "E"

TAARIFA FUPI ZA MIRADI ILIYOPITIWA NA MBIO ZA *MWENGE WA UHURU* 2019.

Wilaya ya Bahi ni moja kati ya Wilaya saba za Mkoa wa Dodoma, ikiwa na Tarafa 4, Kata 22, Vijiji 59, vitongoji 553 na eneo la kilometa za mraba 5,948. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ina jumla ya watu 221,645 (wanaume 105,975 *(47.8%)* na wanawake 115,670 (*52.2%).*Kwa maoteo ya mwaka 2017, Wilaya inakadiriwa kuwa Na watu 245,958 (wanawake 128,358, wanaume 117,600).

Uchumi wa Wilaya unatokana na kilimo na ufugaji. Makadirio ya pato la mkazi Kwa mwaka 2007 yalikuwa sh.206, 000.00, Kwa sasa inakadiriwa pato hili kuongezeka hadi kufikia sh.427, 489.00 sawa na ongezeko la 207.5%.

Miradi itakayopitiwa Na *Mwenge waUhuru* 2019 ni kama ifuatavyo:-

1. TAARIFA FUPI YA MRADI WA UTUNZAJI WA CHANZO CHA MAJI NA UHIFADHI WA MSITU WA ASILI WA CHENENE KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE UHURU KITAIFA 2019.

UTANGULIZI

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

Msitu wa chenene una ukubwa wa hekta 27,628 na umehifadhiwa kisheria kwa tangazo katika gazeti la serikali namba 382 la tarehe 12/05/1989.Msitu huu unamilikiwa na serikali kuu na usimamizi wake uko chini ya wakala wa huduma za misitu Tanzania (TFS)

Msitu huu una umuhimu mkubwa sana kwa kuwa ni moja wapo wa vyanzo vikuu vya maji yanayotumika kwenye Jiji la Dodoma. Kwa ujumla msitu huu ambao umehifadhiwa kisheria umekua na uvamizi wa shughuli za kibinadamu kama ufugaji na uchungaji wa mifugo ndani ya hifadhi ambapo imeonekana kuwepo kwa makundi ya mifugo,ujenzi wa maboma ndani ,makazi na kilimo kinachofanyika kwa kufyeka msitu.

Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na jiografia ya msitu huu ,kuwa karibu na jiji la Dodoma imekua ndio kimbilio la watu wengi kujipatia huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuni ,mkaa, nguzo, fito, mbao, malisho ya mifugo na nyasi za kuezekea nyumba ambazo ni kinyume na uwepo wa hifadhi hii hapa jijini Dodoma.

Pamoja na hayo jiji la Dodoma limepokea wageni wengi wakati huu ambapo serikali inahamia Dodoma, kutokana na hali hiyo kuna kila sababu ya kulinda chanzo hiki kikubwa cha maji ili kuweza kukidhi mahitaji hayo makubwa yaliyopo na yanayotarajiwa kwa kutumia wadau mbalimbali.

LENGO LA KUHIFADHI MSITU

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Lengo la kuhifadhi msitu huu ni kuuhifadhi uoto wa asili pamoja na kutunza chanzo cha maji katika bonde la Mzakwe ambalo linalisha Jiji la Dodoma na baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Bahi .
shughuli za uhifadhi kupitia visiki hai kutoka kwa "Championi wa Lead Foundation", pia viongozi wa Serikali za vijiji waweze kutunga sheria ndogondogo za kutunza mazingira) na kikundi cha ufugaji nyuki ambacho kinasimamiwa na TFS kina jiwezesha kiuchumi na kusaidia kulinda msitu huu.

GHARAMA ZA MRADI

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Mradi huu wa Uhifadhi wa msitu wa Chenene umegharimu kiasi cha shilingi **27,400,000** kwa kikundi cha **Wana Champion wa Lead Foundation** 137 (ambao walipata elimu ya uhifadhi wa mazingira ili waisambaze kwa jamii) ambapo kila mwanakikundi alipewa simu I yenye thamani ya shilingi 200,000/= kwa ajili ya mawasiliano na kutoa taarifa za uharibifu wa mazingira .

CHANGAMOTO NA NJIA ZA KUKABILIANA NAZO

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Mradi unakabiliwa na changamoto ya wanachampioni kuendelea kujitoa bila taarifa na wakati mwingine kuondoka na vifaa (simu).Aidha;Elimu ya uzalendo inaendelea kutolewa kwa jamii ili kulinda na kutunza maliasili za nchi

HITIMISHO

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Tunakuomba sasa ukague na utembelee hifadhi ya Msitu wa Chenene Magharibi kijiji cha Mayamaya.

2. TAARIFA YA MRADI WA UMALIZIAJI WA VYUMBA VINNE VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI YA MUNDEMU KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2019

UTANGULIZI

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Mradi huu wa ujenzi wa madarasa manne (4) Mundemu sekondari ulianza mwaka 2005 kwa michango ya wananchi ikiwa ni jumla ya shilingi **30,000,000/=**. Madarasa yalijengwa mpaka kufikia hatua ya lenta kwa gharama ya shilingi **7,500,000**/= kwa kila boma. Fedha za umaliziaji wa madarasa manne Jumla ya Tsh. 50,000,000 zilitolewa na serikali kupitia mpango wa Ukamilishaji maboma ya vyumba vya madarasa.

LENGO LA MRADI
Lengo la mradi ni kuboresha mazingira ya wanafunzi kujifunza kwa kuwa na madarasa ya kutosha.

GHARAMA ZA MRADI

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Mradi umegharimu jumla ya shilingi **80,000,000**kwa madarasa mannne (4) ikiwa kila darasa ni shilingi **20,000,000** na ujenzi wa vyumba vyote umekamlika umekamilika kwa 100% pamoja na samani zake.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
Kwa heshima na taadhima tuanakuomba sasa uweze kuzindua mradi wetu .

Vyumba vinne vya madarasa shule ya sekondari Mundemu

3. TAARIFA FUPI YA KIWANDA CHA KUZALISHA KOKOTO

KAMPUNI YA KASCCO MUNDEMU

UTANGULIZI:

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mnamo mwezi Aprili, 2019 tulianza kutafuta eneo kwa ajili kuanzisha kiwanda hiki cha Uzalishaji wa kokoto na kufanikiwa kupata eneo katika kijiji cha Mundemu kupitia ofisi za Madini Kanda ya Kati. Tarehe 09 Mei, 2017 ofisi ya Madini Kanda ya Kati walitupatia jumla ya Hekta 55.28.

Mazungumzo na Serikali za Vijiji husika yalifanyika na kukubaliana, hivyo kuanza maandalizi ya kusafisha eneo pamoja na kujenga Karakana, Ofisi, nyumba moja ya kuishi na vyoo. Ilipofika Januari, 2018 tulianza ujenzi wa sehemu za kusimika mitambo, baada ya kupitia changamoto mbalimbali, Aprili, 2019 tulianza Rasmi zoezi la kufunga mtambo, kazi ambayo mpaka sasa inaendelea; Mradi unategemewa kukamilika Oktoba, 2019.

LENGO LA KUANZISHA MRADI:

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Kampuni iliamua kuanzisha Mradi huu katika mkoa wa Dodoma baada ya Serikali kutangaza uhaba wa upatikanaji wa kokoto katika mkoa wa Dodoma kutokana na kuongezeka kwa kasi ya ujenzi katika Jiji la Dodoma na kuwataka wafanyabiashara kuja kuwekeza Dodoma. Hivyo tuliona ni fursa ya kuwekeza na kuchangia Uchumi wa taifa.

MANUFAA YA KIWANDA

Kiwanda hiki kina faida nyingi zikiwemo:-

- Kutoa Ajira kwa Wakazi wa Vijiji vya Mundemu, Chilungulu na Vijiji jirani pindi Mradi utakapokamilika.
- Kujenga Shule mpya katika Kijiji cha Mundemu; kama CSR ya miradi ambayo ipo katika makubaliano.
- Kujenga Zahanati ndogo katika Kijiji cha Chilungulu kama CSR ya mradi.
- Kuongeza Mapato ya Halmashauri kutokana na ulipaji wa "Service Levy" na ushuru.

GHARAMA:

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mradi unategemea kugharimu jumla ya Shilingi billioni tano (5,000,000,000) utakapokamilika.

Kiwanda cha uzalishaji kokoto Kampuni ya KASCCO Mundemu

4. TAARIFA YA UJENZI WA MRADI WA USAMBAZAJI MAJI KIJIJI CHA MKAKATIKA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA *MWENGE WA UHURU* KITAIFA MWAKA 2019

UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

Kijiji cha Mkakatika kipo katika kata ya Mpamantwa, Tarafa ya Bahi Wilayani Bahi. Kijiji kina Vitongoji **9**, idadi kaya **967,** wakazi **4,457** kati yao wanawake **2,306**, wanaume **2,151**.

UJENZI WA MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

Ujenzi wa mradi huu wa maji unategemea chanzo cha maji ambacho ni kisima kirefu klichopo hapa kijijini. Kisima hiki kilichimbwa mwaka 1985, kina urefu wa mita 120 na uwezo wa kuzalisha **lita 12,000** kwa saa. Kwa sasa kisima hiki pia ndicho kinachotumika kutoa huduma ya maji kwa mji wa Bahi.

Ujenzi huu unahusisha kazi zifuatazo:-

- Ujenzi wa vituo **12** vya kuchotea maji.
- Ujenzi wa mlambo **mmoja** wa kunyweshea mifugo.
- Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa **lita 135,000**.
- Ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kusukuma maji (Pampu na paneli za nishati ya jua)
- Ulazaji na ufungaji wa mtandao wa mabomba **mita 28,435**

Kazi zilizofanyika mpaka sasa ni kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa vituo **11** vya kuchotea maji umekamilika.
- Ujenzi wa mlambo wa kunyweshea mifugo unaendelea.
- Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji umekamilika.
- Ulazaji na ufungaji wa mabomba njia kuu ya maji kutoka kisimani mpaka kwenye tenki umbali wa mita **1,985** umekamilika.
- Ulazaji na ufungaji wa mtandao wa mabomba katika njia za usambazaji unaendelea ambapo mpaka sasa vituo **5** kati ya vituo **12** vimeunganishwa na vinatoa huduma ya maji.

Kazi ambazo hazijafanyika ili kukamilisha mradi ni kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa kituo kimoja kwa Ndekwa (DP Na.5)
- Umaliziaji wa mlambo wa kunyweshea mifugo.
- Ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kusukuma maji (Pump na paneli za nishati ya jua).
- Umaliziaji wa mtandao wa mabomba ya usambazaji wa maji ili kuhudumia vituo **7** vilivyobaki.

LENGO YA MRADI

Lengo la mradi ni kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Kijij cha Mkakatika ambao wapo 4,457.

THAMANI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

Ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 31.08.2018, unatazamiwa kukamilika tarehe 29.08.2019 na unatekelezwa na mkandarasi aitwaye **Nipo Africa Engineering Co. Ltd** kwa mkataba wa shilingi **637,897,271.40** fedha ambazo zimeidhinishwa na zitalipwa na Serikali kuu. Mpaka sasa fedha ambazo ameshalipwa mkandarasi ni jumla ya shilingi **128,929,600.14** sawa na **20.2%** ya fedha zote za mradi. Fedha zilizobaki kwa ajili ya kukamilisha mradi ni jumla ya shilingi **508,967,671.26** sawa na **79.8**% ya fedha zote za mradi.

Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mpaka sasa imechangia jumla ya shillingi **5,440,320** ikiwa ni kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa mradi. Kwa upande wa wananchi wa kijiji cha

Mkakatika wamechangia jumla ya shilingi **3,209,150** ikiwa ni thamani ya maeneo waliyoyatoa kwa ajili ya ujenzi wa tenki, vituo vya kuchotea maji na miundombinu ya mabomba.

UENDESHAJI WA MRADI WA MAJI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa:

Wananchi wa kijiji cha Mkakatika kwa kuwezeshwa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya, tumeanzisha na kusajili chombo cha watumiaji maji ambacho kinahusisha vijiji vya Bahi sokoni na Mkakatika.

Majukumu ya chombo ni pamoja na kusimamia uendeshaji na matengenezo ya mradi wetu wa maji ili uwe endelevu. Chombo kimeanzishwa na kusajiliwa tarehe 02.02.2018 na kina wajumbe 9, kati yao wanaume ni 7 na wanawake ni 2. Chombo kina akaunti ya maji ambayo hadi sasa ina jumla ya kiasi cha shilingi **Milioni sita (6,000,000**).

MAFANIKIO YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.

Ujenzi wa mradi huu umeleta na utaleta manufaa mbalimbali kwa wananchi wa kijiji hiki ikiwa ni pamoja na kupata kipato kwa kushiriki katika kazi za ujenzi wa mradi, kupungua kwa muda uliokuwa unatumika kufuata maji mbali ambapo kwa sasa vituo vya maji vimesambazwa katika vitongoji vyote tisa (9) vya kijiji cha Mkakatika, kuimarika afya za wananchi, na pia kupata muda wa kutosha kufanya shughuli za maendeleo.

HITIMISHO

Sisi wananchi wa kijiji cha Mkakatika tunapenda kuishukuru serikali kwa kutuwezesha katika ujenzi wa mradi huu mkubwa ambao ukikamilika utakuwa umeweza kututatulia kero ya miaka mingi ya uhaba wa maji safi na salama.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa:

Kwa niaba ya Wananchi wa kijiji cha Mkakatika, ninakuomba sasa uweke jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wetu wa maji.

Tanki la Maji kijiji cha Mkakatika

5. TAARIFA YA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA BAHI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA MWAKA 2019 TAREHE 18/8/ 2019

UTANGULIZI

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ni miongoni mwa Halmashauri zilizowekwa katika mpango wa Serikali wa ujenzi wa Hospitali 67 za Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 ilitengewa na kupokea kiasi cha shilingi 1,500,000,000. Mradi huu ulianza mnamo Februari,2019 na ujenzi unafanyika kwa njia ya **'direct force account'**

LENGO LA MRADI

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Lengo la mradi huu ni kusogeza karibu huduma muhimu za afya kwa wananchi wa wilaya ya Bahi wapatao **247,746.**

HATUA ZA UJENZI

Ujenzi wa majengo saba ya kipaumbele umekamilika kwa **90%**.Majengo hayo ni: Jengo la Utawala,Jengo la wagonjwa wa nje,Wodi ya wazazi,Jengo la kufulia,Jengo la kutunzia dawa,Idara ya mionzi na maabara.

THAMANI YA MRADI

Jumla ya fedha shs **1,475,000,000.00** zimeshatumika, vifaa vyote vya umaliziaji vimekwisha nunuliwa.

NGUVU ZA WANANCHI

Wananchi wa wilaya ya Bahi toka maeneo mbalimbali walijitoa kufanya kazi katika hatua mbalimbali za ujenzi ambazo thamani yake ni shilingi milioni sita na laki tano tu (**6,500,000**).

CHANGAMOTO

- Makadirio ya gharama ya ujenzi yaliyotolewa na OR –TAMISEMI kuwa chini tofauti na uhalisia.
- Kukosekana kwa mhandisi wa ujenzi.

MIKAKATI

- Kuendelea na kazi ya kumalizia hatua za ujenzi zilizosalia ili majengo haya yaanze kutumika mapema iwezeekanavyo
- Halmashauri kuendelea kuwasiliana na OR TAMISEMI kwa ajili ya ushauri na maboresho.
- Halmashauri kuendelea kutafuta wadau wengine wa maendeleo ili kuchangia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.
- Kuendelea kushirikisha na kuhamasisha wananchi kujitoa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Jengo la Hospitali ya Wilaya

6. TAARIFA FUPI YA MRADI WA UJENZI WA BARABARA YA MWANACHUGU - BAHISOKONI KM.2.3 KWA KIWANGO CHA LAMI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA AGOSTI 18, 2019

1. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 kwa wananchi wa Bahi aliahidi kuwajengea barabara za kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 7.5.

Utekelezaji wa ahadi hii ulianza kufanyika mwaka wa fedha 2015/2016, ambapo hadi sasa jumla ya kilometa 2.3 za lami zemejengwa kwa awamu tofauti kulingana na upatikanaji wa fedha,

2. LENGO MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kuboresha miundombinu ya barabara za Bahi mjini kwa kiwango cha lami ili kuleta kivutio kikubwa kwa wawekezaji mbalimbali kuja katika mji wa Bahi pia kuifanya Bahi kukua kiuchumi na Taifa kwa ujumla.

3. GHARAMA ZA MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Katika utekelezaji wa mradi huu,jumla ya Shilingi bilioni 1.42 zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilometa 2.3 kwa awamu tatu tofauti. Katika awamu ya kwanza mwaka wa fedha 2015/2016, kilometa 0.9 zilijengwa katika barabara ya Bahi Mision – Polisi kwa gharama ya Shilingi 471,000,000.00 na mkandarasi kulipwa fedha zote,

Awamu ya pili mwaka 2016/2017 zilijengwa kilometa 0.7 katika barabara ya mkuu wa Wilaya hadi Polisi , pamoja na uboreshaji eneo la ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kwa gharama ya Shilingi 585,000,000.00 na mkandarasi ameshalipwa fedha zote.

Awamu ya tatu imefanyika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo kilometa 0.7 zimejegwa katika barabara ya Mwanachugu – Bahi sokoni kwa gharama ya Shilingi 364,135,542.37. Jumla ya Shilingi 230,100,952.21 zimeshapokelewa na mkandarasi kalipwa Shiillingi 218,566,271.87. Fedha zilizobaki ni fedha za matazamio(retention money). Ujenzi wa barabara hizi umetekelezwa na kampuni ya kizalendo ya Medes Company Limited ya Dar Es Salaam.

4. CHANGAMOTO

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Ucheleweshaji wa uletaji fedha kutoka Mfuko wa barabara kindetendo kinachoweza kusababisha kuwepo na gharama za ujeleweshaji malipo kwa mkandarasi.

5. HITIMISHO

Ndugu.Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Tunaishukuru sana Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania kwa kuwezesha upatikanaji fedha za utekelezaji wa mradi huu

Kwa heshima na taadhima tuanakuomba sasa uweze kuweka jiwe la msingi katika mradi huu wa ujenzi wa barabara za Bahi mjini kwa kiwango cha lami.

Barabara za lami Km. 2.3 mji wa Bahi

7. TAARIFA YA MRADI WA KITUO CHA UKAGUZI WA MIFUGO BAHI KWA MHE KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2019

MALENGO YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Mifugo kwenye eneo la mnada wa Bahi ulilenga:-

i. Kutatua changamoto zilizoanza kujitokeza baina ya Wafanyabiashara wanaosafirisha mifugo hai toka Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwenda Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kupitia mji wa Bahi na Wakulima ambao mashamba yao yako jirani na lilipokuwa pakilio la zamani (karibu na daraja la mto Bubu).

ii. Kuondoa changamoto kwa wafanyabiashara ya mifugo hai kwenye mnada wa Bahi ambao hawakuwa na sehemu ya kupakilia na kushushia mifugo yao.

THAMANI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru;

Mradi huu ambao ujenzi wake ulianza mwezi Novemba, 2018 na kukamilika mwezi Februari, 2019, umehusisha ujenzi wa mazizi manne ya kukusanyia ng'ombe, pakilio, kibanda cha Mkaguzi wa Mifugo na mlambo wa kunyweshea maji ng'ombe . Mradi umejengwa kwa ushirikiano baina ya **Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji** -*Local Investment Climate (LIC)* na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi; ambao hadi kukamilika kwake umegharimu jumla ya Shilingi milioni **33,888,000** .Kati ya fedha hizi,Halmashauri imechangia shilingi **3,888,00** na LIC shilingi **30,000,000**.

MAFANIKIO YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa;

Kukamilika kwa mradi huu:-

i. Kumesaidia kutatua migogoro iliyoanza kujitokeza baina ya wakulima na wafanyabiashara ya kusafirisha mifugo hai.
ii. Kutatoa fursa kwa wajasiriamali kuwekeza kwenye biashara ya kuuza malisho na maji kwa wafanyabiashara wanaosafirisha mifugo hai kupitia kituo hiki.
iii. Kutatoa fursa kwa wajasiriamali kuwekeza kwenye biashara ya kuuza chakula na vinywaji kwa watu wanaotumia kituo hiki.
iv. Kutatoa fursa kwa mjasiriamali kuwekeza kwenye biashara ya kutoa huduma ya **choo na bafu kwa watu wanaotumia kituo hiki.**

MIPANGO YA BAADAE

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa;

Kwa kuwa mradi huu unahusisha mifugo na binadamu ambao wote wanahitaji huduma ya chakula na maji, mipango yetu ni:-

i. Kugawa maeneo kwa wajasiriamali kwenye eneo la mradi ili waweze kufanya biashara ya kukusanya na kuuza malisho na maji kwa mifugo inayoshushwa na kupakiwa kwenye kituo hiki.

ii. Kugawa maeneo kwa wajasiriamali kwenye eneo la kituo ili waweze kufanya biashara ya chakula na vinywaji kwa wafanyabiashara ya mifugo hai na watu wengine wanaotumia kituo hiki.

iii. Kutoa nafasi kwa mjasiriamali aliye tayari ili aweze kujenga na kuendesha biashara ya huduma ya choo na bafu kwenye eneo la mradi.

iv. Kuweka umeme wa jua kwenye kituo ili kuhakikisha usalama kwa watu wanaotumia kituo hiki kwani kitakuwa kinatumika usiku na mchana.

HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa;

Sasa nakuomba uzindue rasmi kituo hiki cha Ukaguzi wa Mifugo kilichopo eneo la mnada wa Bahi kwenye mji wa Bahi.

Kituo cha Ukaguzi wa mifugo